BUKU LA 23
Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb, na Mwezi wenye Furaha wa Historia ya Watu Weusi.

Ninataka tena kuwakaribisha walimu na wafanyakazi wetu kwenye ofisi na majengo ya shule, na kuwashukuru kwa kazi yao ngumu na kujitolea kwao tunapokuwa tukijiandaa kuwarudisha baadhi ya wanafunzi wetu katika majengo ya shule. Nilijivunia kuona wengi wa wafanyakazi wetu wakirudi kwenye majengo ya shule nilipokuwa nikitembelea shule mnamo Jumatano katika "Siku yangu ya Kuwa Nje." Wafanyakazi wetu walihudhuria, na walikuwa tayari kurudi katika majengo ya shule na kumalizia maandalizi ya kuwakaribisha wanafunzi wetu wakirudi katika masomo ya ana kwa ana katika wiki zijazo.

Ninataka kuwapa shukrani maalum walimu wetu wakuu wa ajabu kwa kazi yao ngumu walipokuwa wakiandaa majengo yetu kwa waalimu na wanafunzi kurudi kwa usalama.

Tumekuwa thabiti katika njia yetu inayoongozwa na sayansi na mwongozo kutoka kwa Centers for Disease Control (CDC). CDC imependekeza kwamba shule zinapaswa kufunguliwa tena haraka iwezekanavyo. Sayansi iko upande wetu. Matokeo yao ni, "Kumekuwa na ushahidi mdogo kwamba shule zimechangia pakubwa kwa ongezeko la maambukizi katika jamii." CDC pia imesema kwamba kuendelea kufunga shule "kunaweza kuathiri vibaya maendeleo ya kielimu ya wanafunzi, afya ya akili, na ufikiaji wa huduma muhimu." Ndiposa kuweka jamii yetu salama na yenye afya, tunamkumbusha kila mtu kuwa macho na afuate mikakati ya kupunguza hatari ambayo itapunguza hatari ya maambukizi katika vituo vyetu.

Kuna sababu nyingi sana 'Ninapenda DeKalb,' lakini sana sana ni kwa sababu ya ahadi thabiti ya wafanyakazi na kujivunia wanafunzi wetu. Asante kwa kuchukua hatua za kurudi kwenye ofisi zetu na majengo ya shule, na mwisho kuandaa kurudi kwa wanafunzi wetu. Nyinyi ndio mabingwa wa kweli wa watoto! Asante kwa kuendelea kuwa wazuri wakati wa nyakati hizi zenye changamoto.

Siku ya Kuwa Nje

Nilifurahi kuona baadhi ya nyuso zenu mnamo tarehe 3 Februari katika Shule ya Msingi ya Bob Mathis, Shule ya Msingi ya Dresden, Shule ya Msingi ya Idlewood, Shule ya Msingi ya Rowland, Shule ya Kati ya Columbia na Shule ya Kati ya Henderson.

Nilikuwa na nafasi ya kushuhudia itifaki za usalama wa shule zikitumika, na walimu wetu walipokuwa wakifunza mtandaoni kutoka darasani mwao. Ilikuwa siku nzuri sana. Asante kwa viongozi, walimu na wafanyakazi wa shule hizi sita kwa ukarimu wenu.

Ninataka pia kumshukuru Msimamizi wa Mkoa wa V Dkt. Triscilla Weaver na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Upili ya Southwest DeKalb Dkt. Thomas Glanton na wafanyakazi wake kwa kuruhusu FOX 5 Atlanta na WSB kuzuru shule na kuonyesha itifaki za usalama za shule.

Tunatumaini ripoti ya vituo vipya itapatia familia zetu za DCSD mwonekano wazi wa jinsi tunavyolenga kuwaweka wanafunzi na wafanyakazi wetu salama wakiwa katika majengo ya shule zetu.

**Mikutano ya Mtandaoni ya Town Hall**

Huku familia zetu zikiamua kama kurudi shuleni ndio chaguo sahihi kwao, tafadhali endelea kutembelea tovuti yetu ya kufungua shule tena kwa maelezo muhimu kuhusu masomo ya mtandaoni, usafiri, itifaki za usalama, na zaidi. Tunapanga mkutano mwingine wa Mtandaoni wa Town Hall kwa ajili ya wazazi mnamo Alhamisi, Februari 11, 2021, kuanzia saa 6 p.m. hadi 7 p.m. Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti yetu.

Ninahimiza pia familia zetu kutazama mkutano wetu wa Bodi ya Elimu mnamo tarehe 8 Februari 2021, saa 11:30 a.m. kwa Mkutano wa Mtandaoni wa Mchango wa Jamii. Tutatoa taarifa kuhusu masomo ya ana kwa ana. Unaweza kutazama mkutano huu kwenye kituo 24 katika Kaunti ya DeKalb au kwenye DSTV online.

**Mikakati ya Kupunguza Hatari**

Mikakati tano muhimu ya CDS ya kupunguza zaidi hatari ya maambukizi na maenezi ya COVID-19 shuleni ni:

- Matumizi sahihi na ya mara kwa mara ya barakoa
- Kutokaribiana na watu ikiwa inawezekana
- Kunawa mikono
- Kusafisha na kuua vidudu
- Kuwafuatilia watu waliokaribiana kwa kushirikiana na Bodi ya Afya ya DeKalb

Tunawahimiza wanafunzi kuzoea mikakati hii mipya sasa, ili wakati wanapoanza kurudi shuleni, kuvaa barakoa, kutokaribiana na wengine, na kunawa mikono kuwe jambo la kawaida.

Ijapokuwa kunawa mikono ni njia muhimu ya kukomesha kuenea kwa vijidudu na kupunguza hatari ya kueneza virusi vya COVID-19, kunawa mikono kwa maji na sabuni kwa angalau sekunde 20 au kutumia kieuzi cha mikono kilichotengenezwa kwa pombe kilicho na angalau asilimia 60 ya pombe ikiwa sabuni na maji hazipatikani, hupunguza kuenea kwa vijidudu ambavyo vinaweza kusababisha ugonjwa, kulingana na CDC. Maji moto na baridi huondoa viwango sawa vya wadudu kutoka kwa mikono yako.

Itifaki zote za usalama zinalingana na mwongozo wa afya uliotolewa na CDC na Bodi ya Afya ya Kaunti ya DeKalb ili kupunguza kuenea kwa COVID-19. Kwa maelezo zaidi kuhusu kunawa mikono vizuri, tafadhali tembelea, tovuti ya CDC na kwa mwongozo husika wa Operations COVID-19, tafadhali tembelea https://www.dekalbschoolsga.org/school-reopening/safety-protocol/.

**Mpango Kamili Mkuu**

DCSD imetekeleza mpango kamili mkuu wa kutathmini vituo vyote vya shule na vya usimamizi, na hata pia miundomsingi ili kuunga mkono misheni ya elimu ya Wilaya. Tunawahimiza wanafunzi, wazazi, wafanyakazi na wanajamii kutembelea tovuti na wakamilishe utafiti wa THINK BIG. Tovuti hiyo inaonyesha maelezo ya mpango na mbinu za mpango kamili mkuu. Huku mpango ukiendelea, maelezo zaidi na tafiti za ziada zitapatikana kwa umma.

Tena, asante kwa uvumilivu wenu tunapoendelea kupata njia wakati wa nyakati hizi zisizo na kifani. Ijapokuwa mustakabali haujulikani, nilihimizwa na kile nilichokiona kutoka kwa walimu na wafanyakazi wetu baada ya kufungua tena. Tutaendelea kuweka afya na usalama wa wafanyakazi wetu kuwa kipaumbele chetu nambari moja. Asante kwa msaada wenu na usaidizi unaoendelea. Tuendelee Mbele na Juu!

Shabiki wenu #1,

Bi. Cheryl Watson-Harris